**`MKATABA HUU NI WA UPANGISHAJI KATIKA JENGO LILILOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 94, KITALU "S" BARABARA YA NYERERE JIJINI MWANZA**

**MKATABA HUU UMETENGENEZWA** hapa Mwanza leo tarehe **01/03/2023**

**BAINA YA**

**SEIF STORE CO. LTD WA S.L.P. 10772 Mwanza. Simu 0784 – 259334, 0622 225 225, E- mail: seifstore@yahoo.com**

(Ambaye ndiye mpangishaji), katika Mkataba huu ana nia ya kupangisha

**NA**

**TRANSEC LTD WA S.L.P. 402 Mwanza – Tanzania**

**(TIN NA.133-640-398) VRN:40-029207-I**

Simu No: **+255 282500458, E-mail:accounts@transec-tz**

(Ambaye ndiye Mpangaji) katika mkataba huu ana nia ya kupanga chumba kwa matumizi ya kufungua ofisi, na kwamba Mpangishaji amekubali kumpangisha Mpangaji **TRANSEC LTD_chumba** No.1,3,4,6 kilichopo ghorofa ya TANO(**5**) kwa ajili ya kufungua Ofisi/Biashara kwa masharti yafuatayo:-

1. **KWAMBA**: Imekubaliwa na pande zote mbili kuwa kodi ya pango itakuwa ni Shilingi za kitanzania **MILIONI MOJA LAKI NANE TU** taslimu (1,800,000/=) VAT Exclusive kwa mwezi na ambazo zitalipwa kwa mwaka katika muda miezi 36 Muda wa mkataba huu ni wa miezi 36 (Miaka mitatu) utakaoanza tarehe **01 / 03 / 2023** na kumalizika tarehe 28/02/2026.

2. **KWAMBA**: Mpangaji hataruhusiwa kufanya biashara au shughuli ya aina yoyote kama kilevi kwa maana pombe ya aina yoyote, madawa ya kulevya, nyama ya Nguruwe pamoja na biashara yoyote isiyokubalika kisheria

3. **KWAMBA**: Mpangaji atawajibika kuchangia malipo ya maji, umeme pamoja na service charge kutokana na makubaliano yake (Mpangaji) na Mpangishaji

4. **KWAMBA**: Mpangishaji hatahusika kwa namna yoyote ile kwa usalama wa mali za Mpangaji.

Certified as True Copy of the Original
Mwema Obeid Molla
Advocate, Notary Public & ...
Sign: ...
Date: 01/03/2023

**5.KWAMBA**: Mpangaji atawajibika pia kuweka chumba hicho kwenye hali ya usafi pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo yatokanayo na uharibifu wa matumizi ya chumba.

**6.KWAMBA**: Mpangaji hataruhusiwa kufanya matengenezo "Partition" kwenye chumba husika, isipokuwa partition za aluminiumu tu ndizo zitaruhusiwa na iwapo tu atapata idhini ya maandishi toka kwa Mwenye nyumba. Izingatiwe kuwa partition hazitaruhusiwa kutolewa katika chumba kwa usalama wa jengo na hapata kuwepo na fidia ya aina yoyote ile wakati mkataba utakapo malizika na Mpangaji kuamua kuhama/ kutoka kwenye chumba, partition hizo zimewekwa kwa hiyari ya Mpangaji mwenyewe.

**7.KWAMBA**: Kwa muda muafaka Mpangaji atamruhusu Mpangishaji kufanya ukaguzi katika chumba husika ili kujiridhisha na hali ya jengo lake kwa mujibu wa mkataba huu.

**8.KWAMBA**: Mpangaji atawajibika kukabidhi chumba kikiwa katika hali nzuri na safi mara baada ya muda wake wa upangaji kumalizika, au kulipia gharama za kurejesha chumba katika hali ilivyokuwa wakati alipoanza upangaji wake.

**9.KWAMBA** : Jukumu la usalama wa mali ya biashara ndani ya chumba husika ni la Mpangaji mwenyewe.

**10.KWAMBA**: Hairuhusiwi kumpangisha mtu au watu wengine bila idhini ya maandishi ya **MPANGISHAJI.**

**11.KWAMBA**: Katika kipindi chote cha mkataba huu, sheria, taratibu na kanuni zinazo ongoza upangaji zitatawala mkataba huu.

**12.KWAMBA**: Endapo kutatokea mgogoro wowote katika kutafsiri mkataba huu au utekelezaji wa mkataba huu basi swala hilo litafikishwa katika Mahakama yenye uwezo wa kisheria kushughulikia swala hilo.

**13.KWAMBA**: Mpangaji atatumia chumba husika kwa shughuli iliyoidhinishwa na kukubaliwa kwenye mkataba huu.

**14.KWAMBA**: A.Endapo Mpangishaji atataka kuongeza kodi ya pango, atatoa taarifa ya siku sitini (60) kabla ya kukoma mkataba huu, na endapo hatakuwa na makubaliano husika Mpangaji atalazimika kuondoka kwenye chumba mara tu mkataba wake utakapo kwisha vinginevyo wakikubaliana mkataba mwingine utaandaliwa na kutiwa sahihi na pande zote mqbili.

B.Endapo Mpangishaji Au Mpangaji hatotaka kutoendelea na upangaji au upangishwaji atoe taarifa (notice) ya mwezi mmoja kabla ya mkataba kumalizika mda wake

15.**KWAMBA**: Mkataba huu utakuwa halali mara tu baada ya pande husika kuweka sahihi zao.

**KWA KUTHIBITISHA**: Yote yaliyo tangulia sisi wahusika tunaweka sahihi mbele ya Mashahidi wetu kama ifuatavyo:-

Umesahiniwa hapa Mwanza kwa niaba ya **SEIF STORE CO. LTD**

**Jina:** SEIF SAID RASHID
**Sifa:** MKURUGENZI MKUU
**Anuani:** P.O. BOX 10772 MWANZA
**Tarehe:** 13/02/2023

Umesahiniwa hapa Mwanza na

**Jina:** SAID SEIF SAID
**Sifa:** MANAGER
**Anuani:** P.O BOX 10772 MWANZA
**Tarehe:** 13/02/2023

Umeshuhudiwa na

**Jina:** Heri E
**Sifa:** Wakili
**Anuani:** 202, Mwanza
**Tarehe:** 16/02/2023

Certified as True Copy of the Original
Mwema Obeid Mella
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign: ..........
Date: 01/03/2023

Umesahiniwa hapa MWANZA kwa niaba ya **TRANSEC LTD**

**Jina:** MAGRETH MACHA

**Sifa:** ACCOUNTANT

**Anuani:** P.O. BOX 16

**Tarehe:** 20/02/2023

TRANSEC LIMITED
P.O. Box 16
MWANZA
TRANSEC LIMITED

Umesahiniwa hapa MWANZA na

**Jina:** SIMRAN BHANJI

**Sifa:** ACCOUNTANT

**Anuani:** P.O BOX 16 MWANZA

**Tarehe:** 16.02.2023

Umeshuhudiwa na

**Jina:** Heri E

**Sifa:** Wakili

**Anuani:** 202, Mwanza

**Tarehe:** 16/02/2023

Certified as True Copy of the Original
Mwema Obeid Mella
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths
Sign:
Date: 0/03/2023

# SEIF STORE COMPANY LIMITED

*P.O. Box 10772 Mwanza, Tanzania Tel. +255 28 250 2066 Fax: +255 28 250 0752*
*Mobile: +255 784 259 334, +255 767 259 334, +255 714 357 034 E-mail:seifstore@yahoo.com*

Ref. No: SSC. 2022 TRANSEC LTD / ON 04

Date: 01/03/2023

**CONDITIONS**

TRANSEC LIMITED,
FLOOR NO. 05 ROOM NO 1,3,4&6
P. O. Box 402
MWANZA.

**YAH: KUCHANGIA GHARAMA ZA ELECTRICITY, WATER & SERVICE CHARGES**

Kuanzia kwa mwezi unaombwa kuchangia huduma tajwa hapo juu kama ifuatavyo:-

1. Electricity Tshs. 410,800/= kwa mwezi.
2. Water Tshs. 60,000/= kwa mwezi
3. Service charges Tshs. 200,000/= kwa mwezi

Mchango huu utakuwa unalipwa kila mwanzo wa mwezi. Na niwavyumba Vinne(4)

Nategemea ushirikiano kutoka kwenu.

SAHIHI YA MTUMIAJI: ____________________

MKURUGENZI MKUU